# KUKOMBOA WAKATI NI JAMBO LAMUHIMU KWA KILA MTU ANAYETAMANI KUFANIKIWA KIROHO AU KIMWILI MAANDIKO: MHUBIRI 3: 1 – 11, WAEF. 5: 15 – 17

**UTANGULIZI:**

**KOMBOA** - Nusuru, weka salama – isipotee

- Ni kutumia wakati vizuri ili usipotee, ukuletee mafanikio
- Kujua nyakati na kuzitumia vizuri ni hatua ya kwanza ya mafanikio yetu – **Mith. 6: 6 – 11.**

  Biblia inatuasa kumwendea **chungu** mdudu mdogo anavyozijua nyakati na kuzichacharikia, hana msimamizi lakini anajua, wajibu wake na wakati wa kuufanya - **Anakusanya chakula chake wakati wa mavuno na kujiwekea akiba - kwake hakuna njaa**.

- **Mith. 31: 25 – 27** – Mwanamke mwema **anaucheka wakati ujao** hana wasiwasi kwa sababu ameutumia wakati wake vizuri ni mwanamke chapa kazi, makini ana maandalizi ya kutosha – **Mst. 15: Huamka kabla haujaisha usingizi** huwapa watu wa nyumbani mwake chakula --- ***Mst. 27*** mmewe na watoto humsifu – **mst. 28 – 29** ooh **Haleluya!!!!**

- Watu wengi waliofanikiwa walijua jinsi ya kutunza na kutumia wakati, Biblia inasema **– "kwa kila jambo kuna majira yake na wakati kwa kila kusudi chini ya Mbingu *Mhub. 3: 1* "** Jambo lolote linalofanyika nje ya wakati halina faida huleta majuto, hata mkulima akilima wakati mvua zinaishilia atapoteza mbegu zake bure. **Mst. 11[a] – unasema kila kitu Mungu amekijfanya kizuri kwa wakati wake"** ukiona mtu amefanikiwa katika jambo lolote elewa kuwa anajua kuutumia wakati vizuri.
- ***Waefeso 5:16*** – Biblia inatuagiza kuukomboa wakati maana ukishapita haurudi wala haupatikani tena.

**Kuna mambo mawili (2) katika maisha ambayo ukiyapoteza hutayapata tena:-**

1. **MUDA – LUK. 19: 41 – 44**

- Yesu aliulilia mji, akahuzunikia kwa sababu - hawakujua majira ya kujiliwa kwao, hawakujua yawapasayo kufanya – walikuwa wakisubiri kuharibiwa.

- ***1Nyak. 12: 32 –*** Wana wa Isakari walijua nyakati na yapasayo Israel kufanya wakawa sababu ya usalama kwa watu wao.
- Ukipoteza muda, ukaacha kufanya yakupasayo kwa wakati huo hutaupata tena kabisa

a. **Mfan.** Kupoteza muda wa kufanya kazi wakati una nguvu – ***Yoh. 9:4*** Ukiwa na nguvu chacharika, fanya vitu vya kueleweka, kuna siku utatamani huwezi tena kila mtu ana mchana wake na usiku wake.
- Kupoteza muda wa kusoma wakati ni kijana – ukijiunga na magenge hovyo mabaya au kuolewa/kuoa – fanya vitu muhimu kwanza – ***Mith. 4:13***
- Kupoteza muda wa kusomesha watoto, au kuwawekea akiba wakati una nguvu na uwezo- Elimu ni mtaji na urithi wa mtoto, tanguliza hilo.
- Kupoteza muda wa kujenga nyumba wakati una nguvu na uwezo. Muda ukishapita umepita haurudi tena.

***b.*** **Hata habari ya kuja kwa Yesu kulichukua kanisa**, Mungu ametuachia muda wa kujiandaa, ametueleza na dalili zote za kuja kwake kwamba zitakuwa nyakati za hatari, uovu utaongezeka mno, lakini **watu hawajali, hawako makini kujilinda na kumtafuta Mungu**. Watu wengi sana wataachwa kwa sababu watu hawajali mud**a**. ***Mf. Math. 25:1-13. Math. 24: 36 – 44.***

**<u>2. FURSA – Math. 14: 1 – 12.</u>**

- **Fursa ni nafasi anayoipata mtu kwa neema ambayo hakutegemea**.
- Ukiipata nafasi ukaichezea hutaipata tena
- Binti Herode alipata fursa ya pekee kutoka kwa babaye, angeweza kujipatia utajiri mkubwa sana, sawa na ahadi za babaye, lakini alipoukubali uchochezi wa mamaye **aliambulia kichwa cha Yohana** Mbatizaji. Wako watu wengi wamepoteza fursa zao kupitia uchochezi na udanganyifu wa marafiki au ndugu. ***Mith. 13:20***

- **Wokovu** – Ni fursa ya pekee ambayo Mungu ametupa hatukustahili tumeokolewa kwa neema siyo kwa matendo yetu mema; lakini bado watu wanauchezea – ***Efes. 2: 8 -9, Ebr. 6: 4 – 6.***

- **Ndoa** uliyo nayo ni fursa wako wangapi **hawajaolewa,kazi, huduma,** afya n.k. **Kumb. 8:18**

- Kuna majuto mengi kwa sababu watu wengi waliokuwa na nafasi ya kuandaa maisha yao ya mbeleni wakati wakiwa madarakani au kazini **walikalia starehe** na **mambo yasiyo na maana**, mwisho wanajuta na kulaumu. Nafasi uliyoipata kuna watu wanaitamani kwamba wangekuwa nayo wangefika mbali- usipoitumia vizuri utaijutia baadaye. Nuhu alipiga kelele miaka 100 akisema gharika inakuja wakawa wanamcheka lakini walikufa wote wakabaki watu 8 tu kizazi vikaanza upya. **Mwz. 7: 17 – 24.**
- Uwe makini na fursa uliyo nayo hakikisha unazalisha mema
- Kutokujua thamani ya nyakati kunamfanya mtu awe mjinga na kufanya yasiyompasa, yasiyomletea manufaa – ***Mith. 9:6.***
- Kwa kukosa kujua umuhimu wa muda na fursa watu wengi wamepata hasara na wengine wanajuta wanasema ningejua!! Majuto ni mjukuu.

**<u>Sababu kuu 3 zinazofanya watu watumie muda wao vibaya.</u>**

1. **<u>Kukosa vipaumbele katika maisha - conviction</u>**
   - Mtu anakuwa hana mipango inayoeleweka - **Hana nguvu ya maamuzi ya kupanga- kipi afanye na kipi kingoje –** ukitaka kufanikiwa ni lazima nyakati zote kuangalia vitu na umuhimu wake na kuweka msimamo. **Baada ya kuokoka kipaumbele chetu cha kwanza kinapaswa kuwa Mungu maana ndiye asili ya mafanikio yetu yote** Mungu apewe nafasi ya kutosha katika maisha yetu na kumtiii katika kila jambo***- Math. 6:33, Luk. 21: 34–36.***
- Kamwe mashumbufu ya maisha yasiteke moyo yetu na kuchukua nafasi ya Mungu

2**<u>. Kukosa utulivu katika kusimamia vipaumbele ulivyokwisha anza</u>**
- Mtu anakuwa limbukeni – Anarukia kitu kingine kabla ya alichoanza, kumalizika, anafukuzana na mambo yasiyo na umuhimu wala lazima kwa wakati huo mf. Kuacha kusoma ukaenda kuolewa, kuacha kujenga ukanunua gari kwanza wakati hata pa kupaki huna, kufukuzana na fasheni za vitu – nguo, fanicha, simu, gari n.k.

unavyo vitu unaacha kuendeleza cha muhimu ulichoanza unanunua maadamu ni fasheni mpya n.k.

3. **Kuahirishaahirisha vipaumbele ulivyopanga katika maisha.**

- Hili ni tatizo kubwa – **ngoja nitafanya kesho – nitasoma kesho, nitajenga kesho, nitaomba kesho**- hii kesho imetesa maisha ya watu wengi - watu wanaacha kufanya mambo muhimu leo na uwezo wanao wanangoja wafanye kesho – mwisho wanazeeka, wengine wanakufa na kesho yao – **maji ukiyavulia nguo oga.**

- Mwiko wa Askari katika uwanja wa vita ni kufanya kila jambo kwa wakati akigeuka nyuma anakula mtutu wa bundiki kwa askari mwenzako.
- Tujitahidi sana Wateule kuukomboa wakati ili tupate faida za kiroho na kimwili. Fanya jambo muhimu kwa wakati sahihi.

Mungu akubariki sana Mteule.

***Na***
***Dr. A. L. MWIZARUBI (MRS)***
***SAYUNI EAGT – ARUSHA.***